**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**
**SHULE YA SEKONDARI WERUWERU**


S.L.P. 575
**MOSHI**

Nambari ya simu: 0768315332/0759659681
Email:weruweru23@gmail.com


Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ..................
..................................................................
S.L.P ............................................................
..................................................................

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI WERUWERU HALMASHAURI YA MOSHI MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2022</u>**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika Shule hii ya Sekondari Weruweru mwaka 2022 tahasusi ya .................., Shule ya Sekondari Weruweru ipo umbali wa kilometa kumi (10) kutoka mji wa Moshi. Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi **cha maili sita nauli shilingi mia nne (400)**.Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe **...................** Mwisho wa kuripoti ni tarehe .......................... **Mwanafunzi akichelewa kuripoti ndani ya kipindi hicho nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.**

## A. MAAGIZO YA FEDHA:

Kwa kuwa binti yako anahitaji vitu kadhaa akiwa hapa Shuleni tuma fedha kwa **njia ya benki jumla ya shilingi 170,000/= (laki moja na elfu sabini tuu)kwa jina la Mkuu wa Shule kupitia akaunti namba 40301100091 Weruweru Sekondari** iliyopo **Benki ya NMB** tawi lolote , kumbuka kuandika jina la mwanafunzi, kidato chake na tahasusi (combination ) sehemu ya ujumbe. **FEDHA TASLIMU HAZIPOKELEWI SHULENI**. Mwanafunzi aje na Nakala ya hati ya malipo. **NAKALA HALISI (original Bank pay in slip).**

**Fedha hizo zitatumika kukidhi mahitaji yafuatayo:-**

| | |
|---|---|
| (i) Ada ya Shule kwa mwaka ........................................................ | 70,000/= |
| (Ii)Fedha ya kuweka kwa ajili ya tahadhari ................................ | 5,000/= |
| (Iii)Matibabu ya dharura ............................................................ | 12,000/= |
| (iv)Kitambulisho, nembo ya shati na picha .................................. | 8,000/= |
| (v)Mfuko wa kuboresha elimu ........................................................ | 20,000/= |
| (vi)Mchango kwa ajili ya walinzi, wapishi na wauguzi kwa mwaka 2022.................................................................................. | 30,000/= |
| (vii)Kukodisha godoro kwa mwaka ................................................ | 10,000/= |
| (viii)Ukarabati wa samani .............................................................. | 15,000/= |
| **JUMLA YA FEDHA ZOTE NI ....................................................** | **170,000/=** |

**B.<u>MAAGIZO NA MAHITAJI MENGINE:</u>**

Binti yako aje Shuleni na mahitaji yafuatayo:-

**<u>B.1 SARE ZA SHULE</u>**

(a) Sketi zinazotakiwa ni mbili (02) zenye rangi ya "light blue" (SUIT MATERIAL) yenye "V" shape mbele isiyo ya kubana ndefu yenye kuvuka magoti muundo wa solo. Ili kurahisisha mfanano katika rangi, mshono na ubora wa kitambaa, Bodi ya Shule imeona ni vyema sare hii ishonewe shuleni kwa usimamizi makini kwa gharama ya shilingi Tsh 32000/= (elfu thelathini na mbili) pesa hii itumwe kwenye **A/C No 40301100091 NMB**

(b) Aje na mashati mawili (02) meupe yenye mikono mifupi aina ya "TOMATO"

(c) Aje na sweta "v" –shape shingoni ya rangi ya **dark blue (NAVY)**

(d) Aje na sketi ya Shule aliyokuwa anaitumia akiwa kidato cha nne atakayo vaa wakati Akisubiria kushonewa sare ya Shule.

(e) Aje na soksi nyeupe (white stockings) jozi nne (04), simple shoes nyeusi za kufunika (jozi moja) kandambili jozi mbili, khanga, gauni la kulala, taulo na **Viatu vyeusi jozi mbili visivyo na kisigino, (flat shoes vya kufunga kwa kamba siyo aina ya FACEBOOK).** Ni muhimu kuzingatia hili kinyume na hapo mwanafunzi atarudishwa.

(f) Aje na magauni mawili marefu yanayovuka magoti ya rangi ya "**light blue**" (mshono wa solo yenye mikono mifupi na kola (baby colar) na suruali yake kama nguo za kushindia. **Nguo zingine haziruhusiwi.**

(g) Aje na "truck suit" nyeusi yenye mistari mieupe na raba nyeusi kwa ajili ya michezo (koti la truck suit lisiwe na kofia).

(h)Aje na ''poly-neck'' nyeusi au nyeupe kama ana matatizo ya kifua.

(i) T- shirt ya rangi ya kijivu (180 type ashgrey) kwa ajili ya michezo alipie Tsh elfu kumi (10,000) kwenye A/C tajwa hapo juu atapata t'shirt yenye nembo ya Shule hapa Shuleni.

(j) Aje na hijabu ya rangi nyeupe kwa ajili ya darasani na rangi ya "light blue" kwa ajili ya kuvalia nguo za kushindia. **Hii ni kwa waislamu tu.**

**N.B: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA NGUO ZA NYUMBANI ISIPOKUWA SARE ZILIZO ELEKEZWA.**

**B.2 Mahitaji mengine.**

(a) Madaftari makubwa (counter books yasiyopungua kumi)

(b) Nakala ya cheti cha **kuzaliwa na Result slip ya kidato cha nne.**

(c) Shuka za kulalia mbili (02) , Blanket la kawaida (student size), mto na foronya mbili, chandarua nyeupe ya duara au mstatili na "Bed cover' shuka la kutandika juu ya kitanda moja (01) ya rangi ya "light blue" ili kuleta ufanano.

(d) "Mathematical set", rula ndefu, kalamu za wino za kuandikia, penseli, kifutio, "stepler mashine", "graph pad", na **"scientific calculator"**, kwa wanao chukua mchepuo wa PCB, ECA, EGM, HGE na HGK **(Aina ya calculator ni CASIO fx – 991MS from Thailand)**

(e) Taulo spesheli (pedi).

(f) Sanduku dogo (size ya kati) la bati la kuwekea nguo zake na kufuli lake imara. Asije na "suit case" hatutalipokea. Asije na begi lenye "charge" (USB BAG) saa (electronic watch) au kifaa chochote cha electronics kinachohitaji kutumia umeme.

(g) Alete Rim moja ya karatasi aina ya Rotatrim au dauble A au Top copie au No. 1

(h) Katika vifaa vilivyoainishwa kwa kila mwanafunzi alete kifaa kulingana na mchepuo wake. **(HGE-FAGIO LA BUIBUI, HKL- JEMBE LILILONOLEWA NA MPINI WAKE, HGK- FYEKEO LILILONOLEWA, PCB –FLOOR SQUIZER, EGM -BRASHI LA CHOONI (toilet brush 1).ECA – LONG SCRUBING BRUSH (Scrubing brush ndefu -1 yenye mpini.**

(i) Ndoo moja (01) ya kuchotea maji yenye ujazo wa /lita 10 kwa matumizi yake binafsi.

(j) Kila mwanafunzi aje na fagio mbili (02) fupi za chelewa na brush ngumu (scrubing brush 02) zisizo na mpini **(Tafadhali zingatia ubora)**

(a) kuna mahitaji mengine madogo kama vile mafuta ya kujipaka yasiyo na harufu sabuni n.k ambavyo binti yako atahitaji. Tafadhali usikose kumpa fedha kidogo za matumizi "pocket money".

**<u>TANGAZO KWA WAZAZI.</u>**

i. Hakikisha binti yako amepimwa na daktari na kujaziwa ripoti kwenye **"FORM FOR MEDICAL EXAMINATION"** iliyoambatanishwa. Ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

ii. Soma kwa makini na binti yako sheria za Shule kisha weka saini **HATI YA UTII WA SHERIA** ambayo imeambatanishwa.

iii. Taarifa binafsi (**INFORMATION SHEET**) ijazwe kwa umakini mkubwa ambayo pia imeambatanishwa. Binti yako aje na fomu zote tatu Shule itakapofunguliwa.

iv. Aje na kijiko cha kulia chakula, sahani na kikombe atapata Shuleni.

**SHERIA ZA SHULE /WIZARA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOGIA**

**A.MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

i) Wizi

ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa

iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

Iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v) Kutishiana/Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.

vi) Ni marufuku mwanafunzi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo Shuleni.

vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

viii) Uvutaji sigara.

ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

x) Kupata ujauzito au kutoa mimba.

xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

**xiii) Kuondoka katika eneo la Shule bila kibali cha Mkuu wa Shule/utoro.**

xiv) Kumiliki, au kutumia simu ya mkononi au kukutwa na line ya simu charge, earphones katika mazingira ya Shule.

xv) Kudharau bendera ya Taifa.

xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu. n.k.

xvii Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

xviii) Makosa ya jinai kama kutishia wengine kwa silaha kama kisu au sumu.

xix) Kulala wawili katika kitanda kimoja.

**B.MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUPEWA ADHABU KALI NA MARUDIO YA MAKOSA HAYA YANAWEZA KUSABABISHA KUACHISHWA MASOMO.**

1.Ni marufuku kukanyaga majani katika eneo la madarasa, nyumba za kulala na bwalo la chakula. Ni lazima kutumia njia zilizowekwa tu. (Covered ways) kosa la kukanyaga majani adhabu itatolewa na viongozi wa wanafunzi.

2.Mwanafunzi lazima awe katika mavazi rasmi ya Shule.

a) Siku ya masomo tangu asubuhi hadi saa ya kulala

b) Jumapili saa za sala. Baada ya sala ataruhusiwa kuvaa nguo za Shule za kushindia.

c) Wakati wowote wa kutoka kwa shughuli mbalimbali kama mkutano, matibabu na safarini, sare ya Shule lazima ivaliwe.

d) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo ya mwanafunzi mwingine.

3.Ni marufuku mwanafunzi kujipamba mfano: kutinda nyusi, kupaka rangi kucha kutumia manukato (perfumes, spray, deodorant), kutumia mafuta yenye harufu, kuvaa hereni na kupaka rangi za midomo.

4.Mwanafunzi haruhusiwi kufuga nywele ndefu wala kusuka. Nywele ziwe fupi urefu wa sentimita moja zilizokatwa kwa kulingana ndizo zinazoruhusiwa.

5. Mwanafunzi haruhusiwi kuja Shuleni na vyombo Vifuatavyo: Redio, pasi,"heater', 'thermos, kamera, **SIMU YA MKONONI , LINE YA SIMU**. Hot pot, walk man au kifaa chochote cha muziki, sufuria , kilevi cha aina yoyote, madawa ya kulevya , sukari, majani ya chai, au chakula cha aina yoyote na albamu za picha (photo- album) wipes, jiki na showerjelly.
6. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuingia jikoni bila ruhusa ya Makamu Mkuu wa Shule.
7 Ni marufuku kwa mwanafunzi kuweka chakula cha aina yoyote katika nyumba ya kulala au kabati la vitabu (locker). Kwa hiyo mwanafunzi asije na chakula cha aina yoyote wakati wa kufungua Shule.
8. Wanafunzi wote wanatakiwa waishi na kushirikiana kindugu. Ni marufuku kutumia lugha ya matusi.
9. Ni marufuku kuandika katika vitabu (text books) kuta, milango, viti, madawati, au mbao za matangazo. Adhabu kali itatolewa atakae kikiuka sheria hii.
10. Mwanafunzi anatazamiwa kufanya kila kazi, iwapo ana matatizo ya kiafya mzazi/mlezi atume taarifa ya Daktari kwa Mkuu wa Shule.
11. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie masomo ya Dini yake bila kukosa kama anavyohudhuria masomo mengine. **Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini akiwa hapa Shuleni.**
12. Mwanafunzi haruhusiwi kulala bwenini wakati wa vipindi (1:30 asubuhi hadi 9:30 mchana) wala wakati wa kujifunza (preparation) jioni kuanzia saa 1:30 usiku hadi saa 5:00 usiku.
13. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa darasani saa 5:00 usiku hadi saa 12:00 asubuh.i
14. Haruhusiwi kuja na kifaa chochote chenye ncha kali kama, kisu, bisibisi panga n.k
15. Ni marufuku kubadilisha mtindo wa sketi ya shule aidha kwa kukata au kubana.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na vitu vya kujipulizia, kujipaka au kujifukiza vinavohusiana na imani mfano "anointed water/oil(maji na mafuta yaliyoombewa, chumvi, nk.

## C. <u>MAAGIZO KWA WAZAZI</u>:

Sheria za Shule zimeorodheshwa hapo juu. Wazazi na wanafunzi ni muhimu kusoma kwa uangalifu na kutia saini zenu za makubaliano katika **FOMU YA UTII WA SHERIA** ambayo imeambatanishwa halafu mzirudishe fomu hizo kwa Mkuu wa Shule. Ni dhahiri kuwa wanafunzi watakuwa wanapoteza wakati wao bure kama wasipotaka kufanya kazi zote kwa bidii na kutii sheria za Shule.

### i) <u>WAZAZI WAGENI KUTEMBELEA SHULE.</u>

Wazazi hawaruhusiwi kuonana na watoto wao wawapo Shuleni. Hii itawasaidia kutumia muda wao vizuri zaidi katika kujisomea. Baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kufika Shuleni na kutaka kuwaona wanafunzi na hii huwasumbua na kuathiri utendaji wao kimasomo.
Iwapo kuna umuhimu wa mzazi kufika Shuleni ataonana na uongozi wa Shule.
**Mwanafunzi asifike Shuleni siku za week-end wakati wa kuripoti kwani hatapokelewa.**
**N.B: Shule ina utaratibu wa kuwa na vikao vya wazazi mara moja kwa mwaka hivyo wazazi mtajulishwa tarehe ya kikao.**

ii) **WANAFUNZI KUTEMBELEA NYUMBANI.**

a) Ametumwa /amepelekwa na Shule.

b) Wazazi wake waje kumchukua kukitokea shida kubwa nyumbani mfano kifo cha baba mzazi, mama mzazi au mlezi wake anayetambulika kisheria (wale tu waliojazwa katika taarifa zake binafsi).

iii) Ni lazima waje na barua yenye saini na muhuri wa mtendaji wa Kijiji/Mtaa kudhibitisha tukio hilo.

iv) Mapumziko mafupi ya katikati ya muhula (Mid term break) wanafunzi wanaruhusiwa kwenda nyumbani kwa wazazi au walezi wao wanaotambulika kisheria tu.

**D.BARUA.**

a) Barua zenye habari za msiba zitumwe moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule. Barua hizo ni lazima ziwe na saini na muhuri wa Serikali ya Kijij/Mtaa.

b) Wanafunzi wanaruhusiwa kuandika barua wakati wa saa za mapumziko.

c) Iwapo mzazi hataki binti yake apate barua toka kwa watu fulani, ni vema amwarifu Mkuu wa Shule.

**E.TIBA (MEDICAL ATTENTION):**

a) Meno, macho, masikio, na kadhalika vikaguliwe wakati mwanafunzi akiwepo nyumbani. Mwanafunzi auguapo akiwa Shuleni **atapewa matibabu katika zahanati ya Shule** na kama ni lazima atapelekwa Hospitali ya Mawenzi, St. Joseph au KCMC. Akilazwa mzazi atajulishwa mara moja na Mkuu wa shule kwa njia ya simu au barua. **Zingatia taarifa za ugonjwa/kuugua mtoto wako unazoletewa na uongozi wa shule tu.**

b) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na dawa zake binafsi kwani atahudumiwa katika Zahanati ya shule **lakini ikiwa amepewa dawa na daktari atatakiwa kumkabidhi muuguzi wa shule ambaye atafuatilia matumizi yake.**

(c) Wagonjwa wote ni lazima walale katika zahanati ya shule na siyo bwenini tena kwa kibali cha muuguzi wa shule.

**F. MATUMIZI YA SIMU (TELEPHONE)**

( a) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga simu, kupigiwa simu na kupokea simu.Iwapo kuna jambo muhimu ambalo mzazi/mlezi anataka kumjulisha ataacha ujumbe kwa karani/uongozi wa shule kwa simu na. **0768-315332**.

(b). **NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUJA NA SIMU YA MKONONI AU (LINE) (TELEPHONE) SHULENI:-** Mwanafunzi akikutwa na simu ya mkononi au line atafukuzwa shule.

**G. USAFIRI:**

Mzazi anatakiwa kumsafirisha binti yake wakati wa kuja shuleni na anaporudi nyumbani wakati wa likizo. Ni muhimu fedha za usafiri zitumwe mapema ili usafiri wa pamoja upangwe na shule.

**H. MAHITAJI:**

Shule inajitahidi kuwapa wanafunzi chakula bora na cha kutosha. Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na chakula cha aina yoyote. Wanafunzi wanaruhusiwa kujinunulia vitu muhimu katika duka la shule, lakini binti asipewe fedha nyingi mno kwa ajili ya vitu hivi vya ziada. Siku ya Mahafali shule inatengeneza chakula (maalumu) kwa ajili ya wahusika wote. Wazazi hawataruhusiwa kuingiza chakula wala kinywaji chochote shuleni. Mzazi haruhusiwi kuingiza zawadi yoyote shuleni. Zawadi zozote hazitapokelewa. Wawekeeni watoto wenu zawadi hizo muwakabidhi warudipo nyumbani.

**I. PESA ZA MATUMIZI:-**

Ni wazi kuwa mwanafunzi lazima apewe pesa za matumizi. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kumpa binti yake kiasi cha pesa anunue sabuni, stampu, bahasha na vitu vingine vidogo. Kuna wazazi wanawapa binti zao pesa nyingi mno mpaka inashangaza. Hivi ni kumzoesha mtoto vibaya, husababisha wizi, mashindano, ubaguzi, tabaka, ugomvi na urafiki usio na msingi. Siyo busara kumpa mtoto fedha nyingi mno.

**J. TAARIFA ZA MAENDELEO YA MWANAFUNZI:-**

Kila mwisho wa muhula kila mzazi atapelekewa kimaandishi taarifa ya maendeleo ya binti yake katika masomo, shughuli za nje ya darasa kazi na tabia. Ni muhimu mzazi/mlezi usome taarifa hiyo na kuwasiliana na shule kama kuna agizo lolote.

Tafadhali wazazi someni taarifa hizo na **KUZINGATIA YALIYOANDIKWA KISHA UWEKE SAINI KATIKA HATI YA UTHIBITISHO** na rudisha kwa Mkuu wa Shule kwa njia ya posta. Chunguza taarifa anazokuletea binti yako ambazo hazikutumwa na Mkuu wa Shule kwa makini, nyingine hazina ukweli. Kama kuna taarifa ya ugonjwa au safari ya kimasomo Uongozi wa shule utawasiliana nawe. Mara nyingi wanafunzi wanatoa visingizio vya ugonjwa, safari au "Tuition" ili wapate fedha za ziada kutoka kwa wazazi wao.

**K. MAHAFALI:-**

Siku ya mahafali ya kidato cha sita ni wazazi/walezi **wawili tu** wanaotambulika kisheria wa wahitimu watahudhuria. Wazazi/walezi hao ni lazima waje na kadi zao za mwaliko. Kuhusu chakula na zawadi rejea kipengele (vii) hapo juu na kukizingatia. Upigaji picha siku ya mahafali utafanywa na mpiga picha wa shule peke yake.

**L. WAJIBU WA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI:-**

i) Kutii sheria zote za shule.
ii) Kuhudhuria vipindi vyote vilivyopangwa kwenye ratiba, kufanya mazoezi yote atakayopewa na walimu na kujisomea kwa bidii.
iii) Kushiriki shughuli zote za usafi, utunzaji wa mazingira ya shule, bustani, shamba na miradi mingine ya shule.

**HITIMISHO:-**

Wazazi tunaomba sana tuwe na malezi ya pamoja ili watoto waendelee na wapate kile walichokifuata hapa shuleni Weruweru, yaani **ELIMU** Msisitizo wa Bodi ya Shule ni kwamba kila mwanafunzi anatakiwa kusoma kwa bidii na kufaulu kwa kiwango cha alama 60% au zaidi katika kila somo. Sheria zote hizo zitalenga kumfanya mtoto apate mazingira bora ya kujisomea na hatimaye aweze kufaulu vizuri masomo yake.

**TUNATEGEMEA USHIRIKIANO WENU.**

**MKUU WA SHULE**

**PRESIDENT OFFICE**
**MINISTRY OF REGIONAL ADMINISTRATION**
**AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**

**WERUWERU SECONDARY SCHOOL,**
**P. O. BOX 575,**
**MOSHI.**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical Officer in respect of all form entrants.

Full Name.......................................................................................................
Age...............................................................................................................
Blood count (Red and White) ..............................................................................
Stool Examination............................................................................................
Urine analysis ................................................................................................
Syphilis test ...................................................................................................
T.B. Test .........................................................................................................
Eye Test ........................................................................................................
Ears ..............................................................................................................
Chest .............................................................................................................
Spleen ...........................................................................................................
Abdomen .......................................................................................................

ADDITION INFORMATION: e.g. physical or chronic family diseases etc.
.............................................................................................................................................................
..................................................................................

I certify that the above is fit to pursue studies
Signature ....................................................................
Designation ................................................................
Section .......................................................................
Date ...........................................................................

STUDENT: You must bring this completed form when you come to School. No student will be allowed to enroll without certificate of physical fitness.

**HEADMISTRESS**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI**

Shule ya Sekondari Weruweru,
S.L.P. 575,
**MOSHI.**

Tarehe ..........................

**HATI YA UTII WA SHERIA**

Mimi Bwana / Bibi ........................................................................ Mzazi / Mlezi wa ......................................................... nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika Maagizo kwa wazazi na nazikubali Sheria hizo na nitashirikiana na Shule kuona kuwa mwanangu anazizingatia kwa manufaa ya Umma.

Mimi ....................................... Binti wa Bwana / Bibi ................................................ Nimesoma kwa makini Sheria za Shule kama zilivyoandikwa na ninazikubali Sheria hizo. Naahidi kuwa nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa naelimishwa na Umma kwa manufaa ya Umma.

................................................... ..............................................

**SAINI YA MWANAFUNZI** **SAINI YA MZAZI**

**TAREHE** **TAREHE**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**MINISTRY OF REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**
**WERUWERU SECONDARY SCHOOL P.O.BOX 575, MOSHI**

**STUDENT INFORMATION SHEET:-**
(This form is to be completed by form five and student transferred to the school. Parts A, B and C to be completed by the student)

**A: PERSONAL PARTICULARS:**
NAME: ..........................................................................................................................................
DATE OF BIRTH: ............................................................................................................................
TRIBE: ..........................................................................................................................................
RELIGION: ........................................................................ DENOMINATION........................................
FATHER'S NAME: ................................................................ OCCUPATION.........................................
MOTHER'S NAME: .............................................................. OCCUPATION .........................................
GURDIAN'S NAME: ............................................................. OCCUPATION .........................................
NUMBER OF SISTER'S: ........................................................ NUMBER OF BROTHERS ..........................
FARTHER'S TELEPHONE NUMBER: .................................... MOTHER'S TELEPHONE NO ........................
HOME ADDRESS: ............................................................................................................................
ANY PHYISICAL/ MEDICAL DISABILITY ...............................................................................................

**B: SECONDARY EDUCATION:-**
..................................................... SECONDARY SCHOOL: FROM ................................ TO ..............................
..................................................... SECONDARY SCHOOL: FROM ................................ TO ..............................
..................................................... SECONDARY SCHOOL: FROM ................................ TO ..............................

**C: PREVIOUS SECONDARY SCHOOL (IF TRANSFER TO THIS SCHOOL)**
NAME OF THE SCHOOL: ..................................................................................................................
ADDRESS: ......................................................................................................................................
"I CERTIFY THAT THE ABOVE INFORMATION IS CORRECT TO THE BEST OF MY KNOWLEDGE"

| ..................................................... | ..................................................... | ..................................................... |
|---|---|---|
| **DATE** | **NAME OF STUDENT** | **STUDENT SIGNATURE** |

**D: (TO BE COPLETED BY FORM CO –ORDINATOR):**
DATE OF ADMISSION TO THIS SCHOOL ............................................................................................
DATE OF ADMISSION NUMBER .......................................................................................................
ADMISSION NUMBER ......................................................... YEAR ...................................................
FORM ADMITTED ............................................................... YEAR ...................................................
DATE OF LEAVING SCHOOL ..........................................................................................................
HIGHEST FORM REACHED ............................................................................................................
CSEE (FORM IV) EXAMINATION NO ...................................... ......................................................
SIGNATURE OF FORM CO-ORDINATOR ................................... DATE ...............................................
SIGNATURE OF THE HEADMISTRESS ..................................... DATE ...............................................